

Shukrani ni za Allah - Mwema, Mkarimu, Mwenye enzi, Mwenye hikma, Mwenye huruma, Mwenye rehema, aliye wahalalishia waja Wake vilivo vizuri kwa hisani Yake, akawaharamishia vilivo vibaya kwa hekima Yake, akawatosheleza katika alivo halalisha wasihitaji alivo haramisha, akawakifu katika ya kumtii wasihitaji ya kumuasi. Kisha Rehema na amani zimshukie Bwana wetu Muhammad, Nabii asiyesoma wala kuandika, ambaye Mwenyezi Mungu amemtuma na ujumbe wa rehema uliokusanya kila kheri, uliozuia kila shari, ulioruhusu kila la maslahi kwa viumbe na manufaa kwa akili zao na miili yao, ulio kataza kila linalo sababisha madhara na maradhi, pamoja na Aali zake wema watakatifu, na Sahaba zake waliopewa nuru na baraka, na kila aliyewafuata kwa wema hadi Siku ya Malipo.

Baada ya hayo, nasema nimeletewa suali kutoka kwa mmoja wa ndugu watukufu wa

nchi ndugu ya Jamhuri ya Moritania, kuhusu kuvuta sigara na hukumu yake, nalo ni hili hapa kama lilivo katika barua yake:

a) Je, kuvuta sigara ni halali au haramu? Dalili gani za kimaandiko zenye kuonesha hilo?
b) Je, hukumu ya asili katika mti wa sigara ni uharamu au uhalali?
c) Na lau kama kitaongezwa katika mti huo kitu kilichokuwa haramu kwa sababu ya najsi au …? Je, itakuwa makruhi* au si makruhi?
d) Nini hukumu ya mwenye kuharamisha halali au kuhalalisha haramu bila dalili.

Kisha akaeleza baada ya hayo hitilafu ya fatwa za maulama waliowauliza wakiwemo wanaosema sigara ni makruhi na wengine wanaoona ni haramu.

Hivyo, na mimi naomba auni kwa Allah nimjibu juu ya ibara hizo zote kwa kadiri nitakavowahi kukumbuka na wakati utakavo

* Makruhi/makuruhi = lenye kuchukiza, si lazima liwe haramu.

ruhusu, japokuwa kwa ufupisho, maana upanuzi wa majibu ya haya utapelekea kurefusha ambako wakati hautatosha na hali haitaruhusu; na Allah Ndiye Mbora wa kutoa auni na kwa kudra Yake mafanikio hupatikana.

Jawabu ya Ibara ya Kwanza:

Kuvuta sigara ni shari isiyokuwa na kheri, na dhara isiyokuwa na faida, na uharibifu usiokuwa na maslahi. Kuvuta sigara kuna madhara kwa mwili na akili, na mali na kizazi, na kunaharibu dini na utu, bali kunaondosha kheri yote ya maisha; kunachafua utulivu wa maisha na kuyaondolea amani. Ni balaa ambalo mvuta sigara anaitakia nafsi yake, na mauti anayoyaendea kwa miguu yake, na sumu kali anayoitwaa kwa mkono wake akaitia kinywani mwake. Madhara ya sigara ni dhahiri mno hata hayahitaji kubainishwa, na yamethibiti kwa uhakika hata hayahitaji dalili.

Sigara katika Mizani ya Madaktari

Zinatosha kelele za madaktari zilizo zagaa kuonya ulimwengu mzima hatari ya janga hili lenye kuua, ambalo linavuna roho za watu kwa wingi, linabomoa na kuvuruga siha zao, linageuza maisha yao kuwa moto usio vumilika, linaua vipawa vyao na kumaliza nguvu zao. Hakuna wanaopinga hilo miongoni mwa wenye ujuzi wa kidaktari au wenye kusoma yaliyo andikwa na madaktari juu ya hilo. Wangapi kati ya madaktari ncha za vidole vyao zimekaribia kulika kwa kushika kalamu kutangaza maonyo kwa Ulimwengu juu ya matokeo ya hatari hii yenye kuangamiza mimea na vizazi, na kuteketeza watu na mazingira.

Juhudi za mashirika ya afya ya kitaifa na ya dunia nzima zimeungana kubainisha yaliyo gunduliwa na yanayo endelea kugunduliwa siku hadi siku, na saa hadi saa miongoni mwa maafa ya ugonjwa huu sugu. Wala hakuna karibu suala lolote lilo kubalika kwa madaktari wote bila tafauti baina ya muislamu na kafiri, wala baina ya mwema na muovu, wala baina ya

aliye salimika nalo na ambaye ana mtihani nalo kama suala la kuvuta sigara na madhara yake kwa anayevuta na asiyevuta, na kujitokeza athari yake kwa binaadamu na mazingira, hata imekuwa lau yangekusanywa yaliyo andikwa juu ya jambo hilo yangetosha peke yake kujaza maktaba kuu kadha.

Kwanitosha kuonesha kwa ufupi yaliyo tolewa na Shirika la Afya la Dunia, na yaliyo tokana na mikutano na semina mbali mbali za kiafya na za kimazingira, na maandishi yaliyo tayarishwa na madaktari mahiri walio isoma hatari hii kwa makini, kama Dakta Muhammed Ali Al-Bar, Dakta Nabil Subhi A'Tawil, Dakta Salama A'Saqaa, Dakta Usama Amin Al-Khauli, Dakta Fadhil Hasan na wengineo; mbali yaliyo andikwa kwa lugha nyengine tafauti zisizo Kiarabu.

Maafa ya Sigara

Sikusudii hapa kutaja madhara yote ya sigara yanayo angamiza na maradhi yote yanayoua yanayo sababishwa na janga hili, maana hilo litapelekea jawabu hii kuwa kitabu kikubwa sana. Inanitosha kusema kuwa kuvuta sigara maafa yake huenea katika seli zote za mwili wa mvuta sigara mpaka haibaki sehemu yo yote mwilini mwake isipokuwa hukumbwa na maafa haya. Kwa ajili hiyo sigara husababisha madhara kwa nguvu zote za mwili na hudhoofisha vipawa vyote vya kinafsi na vya kiakili. Yakutosha yaliyokuja katika kitabu kiitwacho "*A'tad-khin, Al-qalb, Al-jins*" (Sigara, Moyo, Ngono) cha Dakta *Doweranka Eknasova* kwamba kiwango anachovuta mvuta sigara wa wastani kwa muda wa miaka thalathini kina gramu mia nane za kemikali iitwayo nikotini, ambayo inatosha kuutia sumu mji wenye wakaazi alfu kumi.

Hata hivyo kitu hicho si sumu pekee iliyomo katika sigara, bali mna sumu nyinginezo zisizo pungua kuliko hiyo kwa

madhara na maangamizo, kama walivyo bainisha madaktari.

Uorodheshwaji wa magonjwa yote yatokanayo na sigara yaliyotajwa na madaktari japo kwa majina tu bila maelezo unahitaji utungiwe peke yake kitabu kizima. Yatosha kwa mwenye akili kama ni sababu ya kuchukia sigara kuwa aina kadha za maradhi yanayoua ya saratani (kansa) husababishwa na sigara; mbaya mno kati yake ni saratani ya mapafu, na hili hakuna wanaopinga. Vile vile aina kadha za kuvilia damu ('*blood clot*' au '*thrombosis*') zenye kuangamiza zinatokana na sigara; kati yake ni kuvilia damu mishipa ya moyo ('*coronary thrombosis*').

Kuvuta sigara kunaathiri viungo vyote vya usagaji chakula kuanzia mdomo pamoja na kila kilichomo mpaka tumbo, chango, ini na penkriasi. Vile vile kunaathiri viungo vyote vya pumzi kuanzia pua hadi mapafu; na miongoni mwa athari zake ni saratani ya mapafu – kama ilivyo tangulia – na kifua kikuu (TB). Pia kunaathiri sana viungo vya kuzungusha damu mwilini, tangu moyo mpaka mishipa ya damu;

na miongoni mwa athari zake ni ugonjwa wa shinikizo la damu ('*hypertention*' [*high blood pressure*]). Vile vile kuna taathira hatari sana kwa mishipa ya fahamu, hata hufikia hali ya kupoteza uwezo wa kufanya kazi yake. Pia kuna taathira kwa viungo vya mkojo; kati yake ni ugonjwa wa mafigo pamoja na hatari kubwa ya ugonjwa huo. Aidha kunaathiri vibaya misuli na tezindani ('*endocrine glands*'), kama tezi pituitari ('*pituitary gland*', iliyopo chini ya ubongo), tezi thiroidi ('*thyroid gland*', iliyopo chini ya koo), na tezi adrenali ('*adrenal gland*', iliyopo juu ya figo). Sigara ina taathira mbaya pia kwa hisia tano; kila moja ina sehemu yake katika hatari hii ya kuangamiza.

Na katika athari zake kwa watu wengine wasiovuta, sigara ni miongoni mwa vinavyo teketeza kizazi, kwa kudhoofisha viungo vya uzazi kwa wanaume na wanawake, pamoja na kuathiri usalama wa mimba tumboni. Mara nyingi mimba huwa katika hatari ya kuharibika kwasababu ya sigara, pia husibiwa na maradhi mbali mbali kutokana na uvutaji sigara wa wazazi. Watoto wachanga ambao baba zao au mama zao ni wavuta sigara huwa wamekonda

na dhaifu kwa maafa waliyo sababishiwa na wazazi wao, na huwa katika hatari kubwa mno ya kusibiwa na maradhi kuliko wengine.

Ubaya wa kuvuta sigara hauishii kwa wavuta sigara na familia zao tu, bali hukiuka ukaifikia jamii waliyomo, maana sigara ni adui wa mazingira na usalama wake. Moshi wa tumbaku una zaidi ya vitu alfu tatu vya kemikali, na hupelekea hewa kuingia sumu za namna kwa namna, mfano gesi za '*carbon monoxide*', '*hydrocyanide*', '*acrolein*', '*acetaldehyde*', '*ammonia*' na nyenginezo. Hizo zinatosha – Allah atulinde – kueneza majanga ya kuteketeza uhai kwa kuitia sumu hewa kila pahala. Na huu ni katika uharibifu wa bara na baharini unaoingia katika maana ya kauli Yake Taala:

﴿ ظَهَرَ ٱلۡفَسَادُ فِي ٱلۡبَرِّ وَٱلۡبَحۡرِ بِمَا كَسَبَتۡ أَيۡدِي ٱلنَّاسِ لِيُذِيقَهُم بَعۡضَ ٱلَّذِي عَمِلُواْ لَعَلَّهُمۡ يَرۡجِعُونَ ﴾ الروم: ٤١

{Uharibifu umedhihiri bara na baharini kwa yale iliyo yafanya mikono ya watu, ili Mwenyezi Mungu awaonjeshe baadhi ya

waliyo yatenda huenda wakarejea kwa kutubu} (A'rum: 41)*

Hiyo haikuwa ila mifano tu ya maafa ya kuvuta sigara, na haikuwa ila matone machache kutoka bahari kuu ya yale ambayo madaktari na wataalamu wengineo wameyataja katika maandishi yao. Tumeona inatosha kuyataja kwa ujumla pasina maelezo yake mengi na marefu sana yaliyo miminika kama mito kutoka kwenye kalamu za wataalamu, juu ya kutafautiana kwao katika itikadi za dini na mtazamo wa falsafa ya maisha, kwani yote yanaelekea kwenye bahari kuu na pana niliyo ashiria.

* Kwa maana ya aya za Qur'an kitabuni humu, tafsiri mbili mashuhuri za Kiswahili zimetumika kimarejeo, ingawa baadhi ya mwahala - bila kuathiri maana - mfasiri amefupisha au kuongeza maelezo, au kubadili maneno yenye maana sawa au mpangilio au tahajia (spelling). Tafsiri mbili hizo ni:
(1) Tarjuma ya Quran Tukufu kwa Kiswahili, Sheikh Ali Muhsin Al-Barwani, kwenye Mtandao, tovuti yenye kiungo: http://www.iiu.edu.my/deed/quran/swahili/
(2) Qur'ani Takatifu, Tafsiri ya Sheikh Abdulla Saleh Al-Farsi, chapa: The Islamic Foundation, 1980, Nairobi - Kenya.

Wahanga* wa Sigara

Ikiwa kuvuta sigara kuna athari kubwa kiasi hiki, kiasi gani watakuwa wahanga wa sigara wanaokufa kila mwaka kwa kunywa sumu zake, mbali wanao teseka na maradhi na kusumbuliwa na shida zinazo wakuta kwa sababu ya sigara?

Kwa hakika kiwango cha wahanga wa sigara hakijasimama kwenye mpaka maalumu, bali kinaendelea kukuwa kwa kasi. Katika chapa ya mwanzo ya "*Al-Hadyu A'Sihhi*" (Muongozo wa Kiafya) uliochapishwa na Ofisi ya Mashariki ya Kati ya Shirika la Afya la Dunia ukiwa umeambatishwa na hukumu ya kisharia ya kuvuta sigara, takwimu za wahanga hawa zilikuwa zaidi ya milioni mbili na nusu; mauti yanawaondoa ulimwenguni humu kila mwaka kwasababu ya kutumia kwao sumu hii kali. Na katika chapa ya pili walikuwa zaidi ya milioni nne, wala hapakuwa baina ya chapa mbili hizo

* Wahanga = waliofikwa na maafa wakafa au waathirika ('*victims*').

ila miaka kumi na tatu tu. Maana yake ongezeko la idadi yao katika muda huo lilifikia asilimia sitini (60%). Na hivi karibuni – kabla sijaandika jawabu hii – Kitengo cha Kiarabu cha Shirika la Habari la Uingereza BBC kimetangaza kuwa idadi imepanda hadi kufikia milioni tano, kama ilivyotolewa na tovuti* ya Kitengo hicho katika mtandao wa habari wa Ulimwengu. Na Ofisi Tendaji ya Baraza la Mawaziri wa Afya wa Nchi za Umoja wa Waarabu wa Ghuba imeeleza kuwa nchi za magharibi, zenye kusafirisha nje sumu hizi, fungu lao katika wahanga hao wa sigara ni 30%, wakati fungu la nchi zilizobaki, nazo ni zile ziitwazo Nchi Changa, limefikia 70%, kiwango ambacho kinaashiria hatari kubwa, kwani hakioneshi ila ukosefu wa kuelimika, utovu wa busara na kuto kujali matokeo ya maafa hayo.

Utafiti umeonesha kuwa baada ya muda si mrefu idadi ya wahanga wa sigara Ulimwenguni itafikia kwa kila mwaka watu milioni kumi. Na katika taarifa iliyo chapishwa na Benki ya Kimataifa kutokana na Shirika la

* Tovuti = *'website'*, kwa Kiswahili.

Afya la Dunia chini ya kichwa cha habari "Ustawi wa jamii kiutendaji ni kuzuia kasi ya ueneaji wa mabalaa", kumekuja yafuatayo: "Ukiendelea mtindo wa kuvuta sigara kama ulivyo hivi sasa, inakadiriwa kiasi watu milioni mia tano kati ya wanaoishi leo juu ya uso wa Dunia watakufa kwasababu ya kutumia tumbaku; na zaidi ya nusu ya hawa watakuwa miongoni mwa watoto wachanga na vijana." Vile vile hivi karibuni katika tovuti ya Kitengo cha Kiarabu cha Shirika la Habari la Uingereza BBC, chini ya kichwa cha habari "Kuvuta sigara kwaua watu milioni tano kwa mwaka" yamekuja yafuatayo: "Watafiti katika Kitivo cha Afya ya Jamii cha Chuo Kikuu cha Harvard kilioko Boston wanasema, hakika njia pekee ya kuzuia ongezeko la vifo ni kuboresha viwango vya elimu na njia za kupiga vita uvutaji sigara. Watafiti hao waliangalia wastani wa vifo vinavyo sababishwa na kuvuta sigara katika pande zote za Ulimwengu zikiwemo Nchi Changa, ambako vifo vya sigara vinakadiriwa kiasi watu milioni mia tisa na thalathini (930,000,000) kati ya wavuta sigara bilioni moja nukta moja (1100,000,000) Duniani." Na kwenye taarifa iliyo tolewa na Benki ya Kimataifa

kutokana na Shirika la Afya la Dunia yamekuja yafuatayo: "Kuvuta sigara kunaua kwa mwaka mtu mmoja kati ya kila kumi walio baleghe katika pande zote Ulimwenguni wakati tulio nao. Kufikia mwaka 2003, na labda kabla yake kidogo, kiwango kitakuwa mtu mmoja kati ya kila sita walio baleghe, au vifo milioni kumi kila mwaka - yaani vingi kuliko vinavyo tokana na sababu yo yote nyingine peke yake miongoni mwa sababu za vifo."

Ikiwa sigara ina madhara kiasi hiki kwa nafsi, akili, kizazi na mali, basi shaka gani inabaki katika uharamu wake; kwani kudhuru cho chote kati ya vilivo tajwa ni miongoni mwa yaliyo haramishwa kwa makubaliano ya wote; na kulinda usalama wa hivyo ndiyo msingi mkuu wa Sharia Tukufu na miongoni mwa malengo yake makuu.

Dalili za Uharamu wa Sigara

Kwanza: Katika Qur'ani Tukufu

Maandiko yenye kuonesha hukumu ya sigara na uharamu wa kuitumia ni mengi katika Kitabu cha Mwenyezi Mungu Kitukufu. Maandiko yote yenye kuonesha uharamu wa kujiua, kuiathiri akili, ubadhirifu wa mali na kuua watoto, yanaingia katika dalili za uharamu wa kuvuta sigara baada ya kuthibitika madhara yake kwa hivyo vyote.

Zifuatazo ni baadhi ya dalili hizo katika Kitabu cha Mwenyezi Mungu:

1. Kauli Yake Taala:

﴿ يَٰٓأَيُّهَا ٱلَّذِينَ ءَامَنُواْ لَا تَأۡكُلُوٓاْ أَمۡوَٰلَكُم بَيۡنَكُم بِٱلۡبَٰطِلِ إِلَّآ أَن تَكُونَ تِجَٰرَةً عَن تَرَاضٖ مِّنكُمۡۚ وَلَا تَقۡتُلُوٓاْ أَنفُسَكُمۡۚ إِنَّ ٱللَّهَ كَانَ بِكُمۡ رَحِيمٗا ٢٩ وَمَن يَفۡعَلۡ ذَٰلِكَ عُدۡوَٰنٗا وَظُلۡمٗا فَسَوۡفَ نُصۡلِيهِ نَارٗاۚ وَكَانَ ذَٰلِكَ عَلَى ٱللَّهِ يَسِيرًا ٣٠ ﴾ النساء: ٢٩ – ٣٠

{Enyi mlio amini! Msiliane mali zenu kwa dhulma, isipokuwa iwe biashara kwa kuridhiana wenyewe. Wala msijiuwe. Hakika Mwenyezi Mungu ni Mwenye kukurehemuni. Na mwenye kutenda hayo kwa uadui na udhalimu, basi huyo tutamwingiza Motoni. Na hilo ni jepesi kwa Mwenyezi Mungu} (A'nisaa: 29-30)

Aya hiyo imetaja kwa uwazi uharamu wa kuliana mali bila haki na wa mtu kujiua, vyo vyote kutavyokuwa kujiua huko: kuwe kwa kujitumbukiza kwenye moto au kujitupa kutoka juu au kujiangamiza kwa silaha – kama kujifyatulia risasi au kujichoma kisu – au kula sumu, iwe taathira yake ya haraka au taratibu, kama inavyo onesha hadithi ya Abu Huraira kwa Mashekhe Wawili (Bukhari na Muslim) na wengineo kama itakavyokuja insha Allah. Na kwa ajili hiyo Maulama wa Umma wamekubaliana juu ya uharamu wa kula udongo kwasababu kunapeleka kwenye mauti japokuwa ya taratibu.

Mtu huenda akahoji: vipi andiko hili la Qur'ani liwe dalili ya tuliyo yataja kwani wengi wa wafasiri wamelifasiri kwa maana ya watu

kuuana, ingawa kiwakilishi* cha wasemezwa humo (وَلَا تَقْتُلُوٓاْ أَنفُسَكُمْ) **[Wala msijiuwe]** kinaashiria kuwa inamaanishwa mtu kujiua mwenyewe, na kwamba ashirio hilo halikuwa ila kwa ajili ya kutanabahisha kuwa jinsi ya kibinadamu, kwa maumbile yake ya kuwa na mahusiano ya kijamii, inawajibika kumhifadhi kila mmoja kati yake, maana kila mmoja ni kama jamii kutokana na mahusiano yaliyopo baina yao yanayo waunganisha.

Jawabu ya hoja hii ni kwamba andiko hilo ingawa linatoa dalili ya uharamu wa watu kuuana, lakini kutowa kwake dalili ya uharamu wa mtu kujiua mwenyewe kuna nguvu zaidi na wazi mno; maana dhamana ya mtu juu ya nafsi yake ni kubwa kuliko dhamana yake juu ya watu wengine; na kwa kadiri mtu mwengine anavyokuwa kamhusu zaidi na yu karibu naye mno ndivo dhamana yake kwa mtu huyo inavyozidi. Na miongoni mwa dalili za kwamba katika katazo hili kunaingia kujiua mtu mwenyewe na anastahili onyo liliomo, ni vile

* Kiwakilishi katika nahau ya Kiswahili ya sasa ni "kijina" hapo zamani ("*pronoun*").

Amr bin Al'aas alivo itolea hoja aya hiyo tukufu juu ya usahihi wa alivofanya wakati Mtume – rehma za Allah na amani zimshukie- alipomuuliza sababu ya yeye kuacha kuoga janaba akatosheka na kutayamamu badala ya kuoga kisha akawasalisha waliosali nyuma yake wakati alipokuwa amiri wao katika vita vya Dhaat A'salaasil, ambapo alitoa udhuru wa kwamba alijikhofia nafsi yake kutokana na ukali wa baridi, na kwamba alijua kutokana na aya hiyo tukufu kuwa haikumjuzia kufanya lile ambalo lingemdhuru. Mtume -rehma za Allah na amani zimshukie- akaridhika na hoja yake hii wala hakumgomba, na kwa hiyo hoja hii ikawa na hukumu ya kuwa imetoka kwa Mtume -rehma za Allah na amani zimshukie.

Hata hivyo, mvuta sigara hajiui nafsi yake tu, bali anasababisha vifo vya wengine pia. Maana mvuta sigara ye yote anapenda kupuliza sumu zake penye watu. Haoni vibaya mmoja wao, inapokuwa sigara vidoleni mwake na utamu wa kuvuta umeshamkolea, kuwapulizia watu moshi usoni na kuwapelekea kupaliwa na pumzi hata kama kwenye kikao cha kula au kunywa. Na bila shaka hilo ni katika yanayo

sababisha wadhurike, na huenda ikiwa litaendelea likawaharibia maisha yao, jambo ambalo uchunguzi wa kiafya umelithibitisha. Watu ishirini wasiovuta sigara walikaa na kikundi cha wavuta sigara kwa muda wa saa moja katika chumba kisicho pitisha hewa, tahamaki watu hao ishirini wote ilipochunguzwa damu yao ilionekana gesi ya '*carbon monoxide*' ndani ya mishipa yao ya damu imepanda kama kwamba kila mmoja wao kavuta sigara moja kwa kutia puani moshi wake. Haya yamethibitishwa na Kitengo cha Utafiti wa Ushiriki wa Sigara ('*tobacco addiction*') kilicho chini ya Chuo cha London cha Utibabu wa Nafsi.

Uchunguzi mwengine umeonesha kuwa mtu asiyevuta sigara akikaa na wavuta sigara kumi, moshi anaovuta puani haupungui ule anaovuta mmoja wao. Bali taarifa iliyo tolewa na Ofisi ya Mashariki ya Kati ya Shirika la Afya la Dunia imeeleza kuwa uvutaji sigara wa namna hii una madhara makubwa zaidi. Taarifa hiyo ni kama ifuatavyo: “Pengine katika namna mbaya kabisa za uvutaji sigara ni ile ijulikanayo kama ‘uvutaji sigara wa kulazimishwa’, na

unakusudiwa mtu asiyekuwa mvutaji kuvuta pumzi za moshi wa sigara wa watu wengine bila hiari, iwe ofisini au kwenye vyombo vya usafiri au nyumbani. Mwishoni mwa miaka ya thamanini ya karne iliyopita uvutaji sigara wa kulazimishwa ulikuwa kila mwaka ukisababisha idadi ya vifo baina ya alfu nne na alfu tano huko Marekani, na karibu vifo alfu Uingereza, na vifo mia tano nchini Kanada. Na wanawake wasiovuta ambao waume zao ni wavuta sigara wanasibiwa na saratani ya mapafu kwa asilimia kubwa kuliko wanawake ambao waume zao si wavuta sigara."

Katika taarifa iliyotolewa na Benki ya Kimataifa kutoka Shirika la Afya la Dunia yamekuja yafuatayo: "Kuvuta sigara kunaathiri aidha siha ya wasiovuta. Watoto wanaozaliwa na mama wavuta sigara huzaliwa wakiwa wapungufu wa uzito na hukumbana kwa kiasi kikubwa na matatizo ya pumzi, na huwa katika hatari kubwa mno ya kufa ikilinganishwa na vifo vya ghafla vya watoto wachanga kati ya wanaozaliwa na mama wasiovuta sigara. Vile vile walio baleghe kati ya wasiovuta sigara hukumbana na hatari inayoweza kuwa ndogo

mwanzoni, lakini huzidi kidogo kidogo hata ikawafikisha kwenye ugonjwa unaoua au unao upelekea mwili kupoteza nguvu kwasababu ya kuvuta moshi wa sigara za watu wengine."

Aya hiyo imeonesha pia kuwa kutumia sigara ni miongoni mwa maasi makubwa kutokana na makamio yaliyofuatia katika kauli Yake Taala:

﴿ وَمَن يَفْعَلْ ذَٰلِكَ عُدْوَٰنًا وَظُلْمًا فَسَوْفَ نُصْلِيهِ نَارًا ۚ وَكَانَ ذَٰلِكَ عَلَى ٱللَّهِ يَسِيرًا ﴾ النساء: ٣٠

{Na mwenye kutenda hayo kwa uadui na udhalimu, basi huyo tutamwingiza Motoni. Na hilo ni jepesi kwa Mwenyezi Mungu} (A'nisaa: 30)

Na kila ambalo limekamiwa na kutishiwa adhabu katika Qur'ani au Sunna basi hilo ni kosa kubwa.

2. Kauli Yake Taala:

﴿ وَلَا تُلْقُوا۟ بِأَيْدِيكُمْ إِلَى ٱلتَّهْلُكَةِ ﴾ البقرة: ١٩٥

{...wala msijitie kwa mikono yenu katika maangamivu} (Al-baqara: 195)

Aya hii inaonesha kwa ujumla wa hukumu yake uharamu wa kutumia sigara kwa vile kutumia sigara ni kujitia katika maangamivu. Ingawa aya iliteremka kwa sababu maalumu, haizingatiwi sababu hiyo maalumu madamu tamko lake ni la ujumla.

3. Kauli Yake Taala:

﴿ وَمَن يُبَدِّلْ نِعْمَةَ ٱللَّهِ مِنۢ بَعْدِ مَا جَآءَتْهُ فَإِنَّ ٱللَّهَ شَدِيدُ ٱلْعِقَابِ ﴾ البقرة: ٢١١

{Na anaye zibadili neema za Mwenyezi Mungu baada ya kumfikia basi hakika Mwenyezi Mungu ni mkali wa kuadhibu} (Al-baqara: 211) Namna aya hii inavyo onesha uharamu wa sigara ni kwamba siha, akili, kizazi na mali, vyote ni neema ambazo Mwenyezi Mungu humneemesha amtakaye kati ya waja Wake. Na kila ambaye Mwenyezi Mungu amemneemesha kwa neema anawajibika kuitunza na kuto kuifuja, maana kuifuja ni kuibadili. Na tishio lilotajwa ndani ya aya ndilo ambalo Mwenyezi Mungu amemkamia kila mwenye kuibadili neema Yake. Je kuna mwenye akili ambaye

baada ya yaliyo tangulia yote atakuwa na shaka kuwa kuvuta sigara ni kuzibadili neema hizo na kuzifuja?

4. Kauli Yake Taala:

﴿ وَلَا تُؤۡتُواْ ٱلسُّفَهَآءَ أَمۡوَٰلَكُمُ ٱلَّتِي جَعَلَ ٱللَّهُ لَكُمۡ قِيَٰمٗا ﴾ النساء: ٥

{Wala msiwape wasio na akili (ya kuchunga mali) mali zenu ambazo Mwenyezi Mungu amejaalia zikukimuni} (A'nisaa: 5)

Wengi wa wafasiri wameifanya aya hii dalili ya kuto kujuzu kumwachia mfujaji mali aifuje mali yake na kuipoteza, kwa vile ufujaji mali ni kinyume na uwekevu ambao ndio sharti la yatima kuachiwa mali yake baada ya kubaleghe, kwa kauli Yake Taala:

﴿ فَإِنۡ ءَانَسۡتُم مِّنۡهُمۡ رُشۡدٗا فَٱدۡفَعُوٓاْ إِلَيۡهِمۡ أَمۡوَٰلَهُمۡ ﴾ النساء: ٦

{Mkiwaona ni wekevu, basi wapeni mali yao} (A'nisaa: 6)

Na kwa hiyo uhusisho wa kiwakilishi katika neno 'mali' kwa wanao semezwa katika aya hiyo **[msiwape ... mali zenu]** ni kwa ajili ya yale yaliyo tangulia kutajwa ya kwamba umma unapaswa uwe kitu kimoja katika mshikamano wake na mashirikiano yake, kila mmoja achunge

maslahi ya mwenzake kama anavyochunga maslahi ya nafsi yake; kwasababu ingawa kila mmoja anamiliki mali yake peke yake, lakini jamii kwa namna inavyo ingiliana huathirika kwa khasara inayompata ye yote kati ya wanajamii. Na nani anayedai mvuta sigara si mfuja mali. Mwaonaje lau mmemkuta mtu havuti sigara katu, lakini huchukua mwisho wa kila mwaka katika mali yake kiasi cha pesa anazo tumia mvutaji katika sigara akazichoma moto pesa hizo, je huyo ataambiwa mzima wa akili na alilofanya zuri?, juu ya kuwa hakuharibu ila kiasi hicho cha mali; kwani hakuidhuru siha yake wala siha ya mwengine, tafauti na mvuta sigara, ambaye huchoma kiasi hicho cha mali ili ameze sumu zinazomharibia maisha yake, kisha huzitawanya hewani katika mazingira yake ayachafue na kuwadhuru watu ambao idadi yao haina hisabu?

Isitoshe, kama jambo hili lina maslahi kiuchumi, ni ya nani maslahi hayo unadhani? Nani mwenye kufaidika na usafirishaji wa mabalaa haya kuyapelekea mataifa na nchi nyingine? Hapana shaka mfaidika wa mwanzo ni Uzayuni (Utawala wa Kiyahudi) wa Dunia,

ambao mapato yao ya kifedha yanaongezeka kwa kadiri sumu hizi wanazo safirisha nje zinavo tumika. Na kwa kadiri mapato yao yanavo ongezeka ndivo na wao wanavozidi ukatili juu ya umma wa Kiislamu na ukiukaji mipaka katika kuwaua Waislamu, maana ongezeko la mapato yao ndio kuni za moto wa fitna yao. Hii ni kwasababu aghlabu ya mashirika yanayo tengeneza tumbaku ni katika taasisi za kiyahudi.

Nimesoma kabla ya miezi kadha kuwa moja ya mashirika haya makubwa kabisa linatia faida kila mwaka ya zaidi ya dola bilioni mia ($100,000,000,000) ili ziwe silaha mkononi mwa Uzayuni wa Dunia dhidi ya umma huu. Na kutoka wapi fedha hizi humiminika unadhani?! Huo ni utajiri wa umma huu unaofujwa na wavuta sigara kwa ajili ya kushibisha hamu yao ya kuvuta, licha ya matokeo yake ya kupoteza afya yao na kuteketeza nafsi zao. Yale ambayo si milki ya Uzayuni kati ya mashirika haya yanamilikiwa na mama wa Uzayuni na mlezi wake – 'Uwanavita vya Msalaba wa Dunia', ambao unasimama bega kwa bega na Uzayuni katika kuupiga vita Uislamu.

5. Kauli Yake Taala:

﴿ وَلَا تُبَذِّرْ تَبْذِيرًا ﴿٢٦﴾ إِنَّ الْمُبَذِّرِينَ كَانُوا إِخْوَانَ الشَّيَاطِينِ وَكَانَ الشَّيْطَانُ لِرَبِّهِ كَفُورًا ﴿٢٧﴾ ﴾ الإسراء: ٢٦ – ٢٧

{...wala usitumie ovyo kwa ubadhirifu. Hakika wabadhirifu ni ndugu wa Mashetani. Na Shetani ni mwenye kumkufuru Mola wake} (Al-israa: 26, 27)

Namna aya hii inavyo onesha hukumu ya uharamu wa sigara ni kule kuwa ina katazo la ubadhirifu wa mali; na katazo ni dalili ya uharamu. Pia kwasababu imetaja wazi kwamba wabadhirifu ni ndugu wa mashetani; na amali ya shetani ni haramu. Vile vile imebainisha kuwa shetani ni mwenye kumkufuru Mola wake; na maana yake mbadhirifu ni mwenye kukufuru neema ya Mola wake. Na je imebaki shaka yo yote kuwa mvuta sigara ni mbadhirifu wa mali yake baada ya yote yaliyo tangulia?

6. Kauli Yake Taala:

﴿ وَكُلُوا وَاشْرَبُوا وَلَا تُسْرِفُوا إِنَّهُ لَا يُحِبُّ الْمُسْرِفِينَ ﴾

الأعراف: ٣١

{...na kuleni na kunyweni, na msitumie kwa fujo. Kwa hakika Yeye hawapendi wanao tumia kwa fujo } (Al-a'raaf: 31)

Namna aya hii inavyo onesha uharamu wa sigara ni kwamba Mwenyezi Mungu S.W. amekataza kutumia kwa fujo - nako ni kukiuka mipaka ya wastani – hata katika kula na kunywa, juu ya kuwa mawili haya mwili hauna budi nayo. Na Maulama wamekataza kwasababu ya aya hii mtu kula kitu baada ya shibe wakalihisabu hilo kama haramu kwa kuwa linaingia katika utumiaji kwa fujo, halikadhalika kunywa baada ya kukata kiu. Ikiwa hayo ni kuhusu chakula na kinywaji pamoja na raha na ladha iliyomo, na juu ya kuwa viwili hivi ni miongoni mwa vitu muhimu kabisa na vya lazima kwa uhai, basi kefu kutumia mali katika sigara, yenye kudhuru mwili, akili, mali, kizazi, mtu binafsi, jamii, binaadamu na visivokuwa binaadamu?

7. Kauli Yake Taala kuhusu waja wa Rahmani:

﴿ وَٱلَّذِينَ إِذَآ أَنفَقُواْ لَمۡ يُسۡرِفُواْ وَلَمۡ يَقۡتُرُواْ وَكَانَ بَيۡنَ ذَٰلِكَ قَوَامٗا ﴾ الفرقان: ٦٧

{Na wale ambao wanapo tumia hawatumii kwa fujo wala hawafanyi ubakhili, bali wanakuwa katikati baina ya hayo} (Al-furqan:67)

Namna aya hii inavyo onesha hukumu hiyo ni kwamba utumiaji wa fujo si katika sifa za waja wa Rahmani, ambao watalipwa mabustani yaliyo juu kwa juu kwa kuwa na subira; bali ni tabia ya walio kinyume nao ambao ni wafuasi wa Shaitan. Na imebainika kwa namna isiyokuwa na shaka kwamba kutumia pesa katika sigara ni ufujaji mali, maana ni kuharibu mali katika lile ambalo linadhuru halinufaishi, na lina khasara halina faida.

8. Kauli Yake Taala kuhusu Mtume Wake – rehma za Allah na amani zimshukie:

﴿ وَيُحِلُّ لَهُمُ ٱلطَّيِّبَٰتِ وَيُحَرِّمُ عَلَيۡهِمُ ٱلۡخَبَٰٓئِثَ ﴾ الأعراف: ١٥٧

{... na anawahalalishia vizuri, na anawaharamishia viovu} (Al-a'raaf: 157).

Sigara ima itakuwa miongoni mwa vizuri ambavyo Mtume –rehma za Allah na amani zimshukie- anavihalalisha kwa amri ya Mola Wake, au itakuwa miongoni mwa viovu ambavyo anaviharamisha. Je mwenye busara na akili atasema sigara ni katika vitu vizuri baada ya kuthibitika madhara yake yaliyotajwa, pamoja na kuwa harufu yake mbovu na ladha yake mbaya, wala haina mwisho mwema ila maradhi, usumbufu na mabalaa?

9. Kauli Yake Taala:

﴿ وَٱلَّذِينَ يُؤْذُونَ ٱلْمُؤْمِنِينَ وَٱلْمُؤْمِنَٰتِ بِغَيْرِ مَا ٱكْتَسَبُوا۟ فَقَدِ ٱحْتَمَلُوا۟ بُهْتَٰنًا وَإِثْمًا مُّبِينًا ﴾ الأحزاب: ٥٨

{Na wale wanao waudhi Waumini wanaume na wanawake pasina wao kufanya kosa lolote, bila shaka wamebeba dhulma kubwa na dhambi zilio dhahiri} (Al-ahzaab: 58)

Hii ingawa iliteremka kwa sababu maalumu lakini sababu hiyo hailifungi neno kuudhi kwa namna moja pekee; na kwa hiyo aya inamhusu kila anayemuudhi muumini mwanamme au mwanamke kwa namna yo yote ile. Kwani kila ambacho hakifai kulifanya tamko la jumla liwe

makhsusi hakifai pia kulifunga tamko huru kwa namna moja pekee. Na miongoni mwa misingi ya Kiusuli mashuhuri kwamba hapazingatiwi sababu maalumu pakiwa na ujumla wa tamko.

Hilo linaungwa mkono na kutiliwa nguvu na hadithi: **"Kila mwenye maudhi atakuwa Motoni".** Na je imebaki shaka kwamba mvuta sigara huwaudhi wengine kati ya waumini wanaume na wanawake na wengineo? Angekuwa hana maudhi isipokuwa kutia sumu mazingira yao na kuchafua hewa yao yangetosha, kwani athari ya hilo hujitokeza kwa watu, wanyama, hata mimea. Yamtosha mvuta sigara katika makosa kuwa anamuudhi mwenye kukaa nae, hajali kumpulizia moshi usoni pamoja na harufu yake mbovu na sumu zake kali, wala habali kama hilo linaweza kumsumbua au kumuumisha kichwa au kumsababishia magonjwa.

Na kama ilivyo tangulia kuelezwa katika Muongozo wa Kiafya ulio chapishwa na Shirika la Afya la Dunia, uvutaji sigara wenye madhara zaidi ni ule wa kulazimishwa. Lakini asiyevuta huenda akalazimika kukaa na mvutaji kwa haja

yake binafsi ambayo hana budi nayo. Isitoshe, maudhi ya mvuta sigara kwa mwenye kukaa nae si wakati anapovuta tu, bali mara nyingi watu anaowakaribia hukereka na harufu mbovu itokayo kinywani na puani mwake, na ambayo huwa kali mno anapokuwa ameshavuta si muda mrefu uliopita. Na pengine huunga safu ya sala akawaudhi walio karibu nae hata akawakosesha unyenyekevu na kuwanyima ladha ya kunon'gona na Mola wao. Mimi binafsi yamenikuta hayo mara nyingi nilipofikwa na mtihani wa mvuta sigara kusimama ubavuni mwangu, zikanishughulisha harufu zilizo nijia kutoka kwake na zikaupeleka moyo wangu mbali na sala mpaka nikatamani sala iwe fupi, kwasababu ninabaki katika hali ya wasiwasi mpaka imamu anapotoa salamu kumaliza sala. Ikiwa Mtume –rehma za Allah na amani zimshukie- amemzuia yule ambaye amekula thomu au kitunguu maji kuukaribia msikiti, juu ya faida zilizomo katika viwili hivyo, basi seuze anayevuta sigara - kitu kiovu! Kisha harufu ya thomu na kitunguu maji ingawa inachukiza lakini haikaribii harufu ya sigara kwa maudhi.

10. Kauli Yake Taala:

﴿ وَإِذَا تَوَلَّىٰ سَعَىٰ فِي ٱلْأَرْضِ لِيُفْسِدَ فِيهَا وَيُهْلِكَ ٱلْحَرْثَ وَٱلنَّسْلَ ۗ وَٱللَّهُ لَا يُحِبُّ ٱلْفَسَادَ ﴾ البقرة: ٢٠٥

{Na wanapo ondoka wanakwenda huku na huku katika nchi kufanya uharibifu humo na kuangamiza mimea na viumbe. Na Mwenyezi Mungu hapendi uharibifu} (Al-baqara: 205)

Namna aya hii inavyo onesha uharamu wa sigara ni kwamba mvuta sigara anafanya uharibifu katika nchi kwa kuchafua mazingira, na kwa hilo anakuwa amechangia katika kuangamiza mimea na viumbe, jambo ambalo limethibitika kitaalamu na habishani juu yake ila mjinga au anayejifanya mjinga.

11. Kauli Yake Taala:

﴿ قَدْ خَسِرَ ٱلَّذِينَ قَتَلُوٓاْ أَوْلَٰدَهُمْ سَفَهًۢا بِغَيْرِ عِلْمٍ ﴾

الأنعام: ١٤٠

{Hakika wamekhasirika wale ambao wamewaua watoto wao kwa upumbavu pasipo kujua} (Al-an-'aam: 140)

12. Kauli Yake Taala:

﴿ وَكَذَٰلِكَ زَيَّنَ لِكَثِيرٍ مِّنَ
ٱلْمُشْرِكِينَ قَتْلَ أَوْلَٰدِهِمْ شُرَكَآؤُهُمْ
لِيُرْدُوهُمْ وَلِيَلْبِسُواْ عَلَيْهِمْ دِينَهُمْ ﴾ الأنعام: ١٣٧

{Na kama hivyo wengi katika washirikina, washirika wao (wanaomshirikisha nao Mwenyezi Mungu) wamewapambia kuwaua watoto wao ili wawaangamize na kuwavurugia dini yao} (Al-an-'aam: 137)

13. Kauli Yake Taala:

﴿ قُلْ تَعَالَوْاْ أَتْلُ مَا حَرَّمَ رَبُّكُمْ عَلَيْكُمْ ۖ أَلَّا تُشْرِكُواْ بِهِۦ
شَيْـًٔا ۖ وَبِٱلْوَٰلِدَيْنِ إِحْسَٰنًا ۖ وَلَا تَقْتُلُوٓاْ أَوْلَٰدَكُم مِّنْ
إِمْلَٰقٍ ۖ نَّحْنُ نَرْزُقُكُمْ وَإِيَّاهُمْ ﴾ الأنعام: ١٥١

{Sema: Njooni nikusomeeni aliyo kuharamishieni Mola wenu. Nayo ni kuwa, msimshirikishe Yeye na chochote. Na wazazi wenu wafanyieni wema. Wala msiwaue watoto wenu kwa sababu ya umasikini. Sisi

tunakuruzukuni nyinyi na wao} (Al-an-'aam: 151)

14. Kauli Yake Taala:

﴿ وَلَا تَقْتُلُوٓاْ أَوْلَٰدَكُمْ خَشْيَةَ إِمْلَٰقٍ ۖ نَّحْنُ نَرْزُقُهُمْ وَإِيَّاكُمْ ۚ إِنَّ قَتْلَهُمْ كَانَ خِطْـًٔا كَبِيرًا ﴾ الإسراء: ٣١

{Wala msiwaue watoto wenu kwa kuogopa umasikini. Sisi tunawaruzuku wao na nyinyi. Hakika kuwaua ni khatia kubwa} (Al-israa: 31) Namna aya hizi zinavyo onesha uharamu wa sigara ni kwamba mvuta sigara anaua watoto wake, ingawa kuua kwake si moja kwa moja. Hilo ni kutokana na yaliyo tangulia kuelezwa ya kwamba kuvuta sigara kwa baba au mama kuna taathira mbaya kubwa kwa mimba na watoto wachanga, inaweza ikapelekea mimba kuharibika na mtoto mchanga kufa, kwasababu watoto ambao wazazi wao ni wavuta sigara wana hatari ya kupata tauni* ya kuwateketeza na maradhi ya kuwaangamiza, mbali ya kuwa dhaifu wa nguvu na ustahamilivu kuliko wengine.

* Tauni = mlipuko wa maradhi yo yote ya kuambukiza yanayo enea kwa kasi.

Wala isisemwe katazo la kuwaua watoto katika baadhi ya aya hizi limeambatishwa na umasikini au khofu ya umasikini na kwa hiyo haikatazwi ila yakiwepo hayo; kwasababu huko ni kuambatishwa jambo na hali zake za aghlabu na kawaida, na kwa hiyo hakulifungi lisihusu hali nyenginezo.

Haya ndiyo niliyowahi kuyakumbuka katika dalili za Qur'ani juu ya kuharamika kwa sigara bila ya kuzitaja zote.

Pili: Katika Sunna Takatifu

Sunna ya Mtume ina dalili nyingi juu ya hukumu hiyo. Kati yake ni zile zilizo tangulia kutolewa hoja wakati wa kubainisha dalili za Kitabu cha Allah. Zifuatazo ni zile ninazo kumbuka kwa wakati huu kati ya nyenginezo:

1) Ametoa Al Bukhari, Muslim na A'Tirmidhi kutokana na Abu Huraira kutoka kwa **Mtume –rehma za Allah na amani zimshukie- kasema:**
"Atakaejitupa kutoka mlimani akajiua, atakuwa kwenye moto wa Jahannamu anaanguka humo kwa kudumu na kudumishwa milele. Na atakaekunywa

sumu akajiua, sumu yake itakuwa mkononi mwake anainywa kwenye moto wa Jahannamu kwa kudumu na kudumishwa milele. Na atakaejiua kwa kisu, kisu chake kitakuwa mkononi mwake anajichoma nacho tumboni kwenye moto wa Jahannamu kwa kudumu na kudumishwa milele." Ameitoa pia Abu Daud kwa tamko lifuatalo:

"Atakaekunywa sumu, sumu yake itakuwa mkononi mwake anainywa kwenye moto wa Jahannamu kwa kudumu na kudumishwa milele."

Namna hadithi hii inavyo onesha hukumu ya sigara ni wazi, maana haikubaki shaka katika nafsi ya mwenye akili kuwa sigara ni sumu kali; haimteketezi mvutaji tu, bali pia na mwenye mtihani wa maudhi ya moshi wake.

2) Amepokea Al Bukhari kutoka kwa Abu Huraira –Allah amridhie- kwamba **Mtume –rehma za Allah na amani zimshukie- kasema:**

“Atakaejinyonga atajinyonga Motoni, na atakaejichoma kisu atajichoma kisu Motoni.”

Na kwa vile kuvuta sigara kunaharibu viungo vya pumzi basi hukumu yake ni kama kujinyonga.

3) Amepokea A’Tirmidhi kutoka kwa Abu Barza Al Aslami Allah amridhie- kutoka kwa **Mtume –rehma za Allah na amani zimshukie- kwamba amesema:**

“Haiondoki miguu ya mwanaadamu Siku ya Kiyama kwa Mola wake mpaka aulizwe kuhusu matano: Kuhusu umri wake katika nini aliumaliza? Na kuhusu ujana wake katika nini aliuchakaza? Na kuhusu mali yake wapi ameichuma na katika nini aliitumia? Na nini alifanya kuhusu ilmu aliyojua?”

Namna hadithi hii inavyo onesha hukumu ya sigara ni kama ifuatavyo:

Mosi: Mja ataulizwa kuhusu umri wake katika nini aliumaliza; kwani hakuumbwa bila lengo, wala hakuachiwa afanye atakavo, bali kaumbwa kwa

shabaha maalumu imeelezwa na kauli Yake Taala:

﴿ وَمَا خَلَقْتُ ٱلْجِنَّ وَٱلْإِنسَ إِلَّا لِيَعْبُدُونِ ﴾

الذاريات: ٥٦

{Na sikuwaumba majini na watu ila waniabudu} (A'dhaariyaat: 56)

Kinaingia katika ibada ya Mwenyezi Mungu kila akifanyacho mtu baada ya kutekeleza fardhi zake kati ya vyenye manufaa kwa nafsi yake au kwa jinsi ya wanaadamu wenzake kama ataitakasa nia yake. Ama akiutumia umri katika yaliyo kinyume na hayo, au akipoteza sehemu ya umri katika uovu, ufisadi na uharibifu, basi atabeba jukumu la hayo mbele ya Mwenyezi Mungu S.W. Mvuta sigara ambaye anapitisha sehemu ya wakati wake katika kuvuta moshi wenye sumu na katika kuidhuru nafsi yake na watu wengine hajaupa umri huu haki yake, bali ameupoteza katika uharibifu na amesababisha kuumaliza.

Pili: Ataulizwa kuhusu ujana wake suala peke yake kwa vile awamu ya ujana ni awamu ya nguvu na ushupavu; kwani

ujana ndio awali na ubichi wa umri, yampasa autunze na autumilie vizuri kwa kuzielekeza nguvu zake kwenye yale ambayo yatamletea manufaa yeye mwenyewe, dini yake na umma wake. Na bila shaka amepoteza ujana wake yule ambaye ameufisidi kwa kutumia sumu hizi zenye kuua.

Tatu: Ataulizwa kuhusu mali yake alivyoichuma na alivyoitumia kwasababu ni mali ya Mwenyezi Mungu Subhana, haijuzu kuipoteza katika yasiyokuwa na faida, kwani yeye hakupewa mali ila iwe amana kwake na yeye awe mwenye dhamana juu ya mali aliyopewa. Kwa hiyo anapaswa aitumie katika manufaa siyo madhara, na katika kuamirisha siyo kudamirisha, na katika kutengeneza siyo kuharibu. Na kwa ajili ya ulazima wa kuihifadhi ametakiwa awe na kiasi katika kuitumia hata katika njia za kheri, itakuwaje akiitoa iwe thamani ya sumu anayojiangamizia nafsi yake na umma wake. **Imekuja katika hadithi:**

"Mwenyezi Mungu amechukia kwenu kusikia uvumi mkauvumisha, na

kukithirisha masuali, na kupoteza mali."

4) Amepokea A'Tabarani kwenye *al-Awsat* kwa njia ya Anas –Allah amridhie- kwa sanadi nzuri kwamba **Mtume –rehma za Allah na amani zimshukie- kasema: "Atakaemuudhi Muislamu ameniudhi, na atakaeniudhi amemuudhi Mwenyezi Mungu"**.
Yamekwisha kuelezwa maudhi ya mvuta sigara kwa Waislamu kwa uvundo wa harufu yake na kuwadhuru wao na mazingira yao, na huko ni kumuudhi Mwenyezi Mungu na Mtume Wake kama inavyo onesha hadithi. Mweyezi Mungu amesema:

﴿ إِنَّ ٱلَّذِينَ يُؤْذُونَ ٱللَّهَ وَرَسُولَهُۥ لَعَنَهُمُ ٱللَّهُ فِى ٱلدُّنْيَا وَٱلْءَاخِرَةِ وَأَعَدَّ لَهُمْ عَذَابًا مُّهِينًا ﴾ الأحزاب: ٥٧

{Hakika wanao muudhi Mwenyezi Mungu na Mtume wake, Mwenyezi Mungu amewalaani duniani na Akhera, na amewaandalia adhabu ya kufedhehi} (Al-ahzaab: 57)

5) **Mtume –rehma za Allah na amani zimshukie- amekataza kila kinacho lewesha na kinacho pumbaza akili, kama ilivyotolewa na Ahmad na Abu Daud kwa njia ya Mama wa Waumini Ummu Salama –Allah amridhie.**
Sigara ikiwa haileweshi inapumbaza akili, na imekwisha kuelezwa taathira yake juu ya mishipa ya fahamu.

6) **Kauli ya Mtume –rehma za Allah na amani zimshukie:**
"Haijuzu kuleta madhara wala kulipana madhara katika Uislamu." Imepokewa kwa sanadi kamili hadi kwa Mtume na kwa sanadi iliyopungua sahaba, lakini njia zake zinapeana nguvu; nayo ni miongoni mwa misingi ya fiqhi iliyokubaliwa na wote. Wala sidhani kama kuna shaka iliyobaki katika nafsi ya mwenye akili kuwa sigara ina madhara makubwa.

7) Hadithi zinazoonesha kamio la mwenye kujiua, kama hadithi ya Jundub bin Abdalla –Allah amridhie- iliyopo kwa

Mashekhe Wawili (Al Bukhari na Muslim) kuhusu mtu aliyejeruhiwa akashindwa kusubiri, akachukua kisu akauchinja nacho mkono wake na damu haikusita mpaka akafa, **Allah akasema: "Mja wangu kaniharakizia nafsi yake na Mimi namharamishia Pepo."**

Pia hadithi ya Abu Huraira na Sahl bin Sa'd A'Saa'idi –Allah awaridhie- iliyopo kwa Mashekhe Wawili kuhusu kisa cha mtu aliyekuwa kapigana sana katika jihadi kuliko watu wengine, akajeruhiwa, akajiua; **Mtume –rehma za Allah na amani zimshukie- akasema kuwa huyo ni miongoni mwa watu wa Motoni.**

Namna zinavyo onesha hadithi hizi hukumu ya sigara ni kwamba kujiua hakuna tafauti baina ya aina zake na jinsi zake kwa njia yo yote itakayo tumika. Bali kujiua kwa namna zote ni haramu, na hiyo ndiyo hatima wa mwenye kufanya kosa hili - Allah atulinde!

Pamoja na hayo, sigara husababisha madhara mengine mengi ambayo hatujayataja. Kati yake ni mvuta sigara kuwa mateka wa tabia

hii mbaya ikawa inamdhalilisha na kumpelekea kufanya mengi kati ya mambo yaliyo haramishwa na yanayo chukiza kwa kushindwa kuachana nayo. Mmoja kati ya washairi ametoa taswira ya hali hiyo ya wavuta sigara katika nusu ubeti aliposema kuhusu sigara:

"Niliitwaa niitumie nikawa naitumikia"

Mvuta sigara hufanya bidii kubana matumizi apate kununua sigara, hata ikiwa kwa kuwabania wanaomtegemea na kuwanyima baadhi ya vitu vusivo budi na vinavo hitajika kwa maisha. Na huenda ikabidi akope bila kubali kujidhalilisha na kuchuna uso wake. Bali hali inaweza kumfikisha katika udanganyifu na hata kuiba. Yote hayo ni katika ambayo Uislamu hauyakubali kwa wafuasi wake.

Uoni wa Wenye Ilmu kuhusu Sigara

Kwa ajili ya haya yote, wenye busara katika madhehebu zote za Kiislamu tangu mwanzo wa kujitokeza tabia hii mbovu katika nchi za Kiislamu wametoa fatwa kuwa sigara ni haramu. Tafauti ya uoni kutoka kwa baadhi ya watu wa fatwa ilitokana na kuto kuelewa ukweli juu ya sigara na madhara yake mengi. Na ikiwa tafauti hii ya uoni juu ya sigara ilienea miongoni mwa aghlabu ya madhehebu za Kiislamu katika zama zilizopita, maulama wa madhehebu yetu hawakutafautiana katu kuhusu suala hili; bali walikubaliana wa mashariki na wa magharibi tangu awali ya kudhihiri janga hili katika nchi za Kiislamu juu ya uharamu wa kuvuta sigara, bali na uharamu wa kutumia tumbaku kwa njia yo yote ile, iwe kwa kunusa puani au kuweka kinywani au kuvuta moshi wake. Na katika mafanikio waliyojaaliwa na Mwenyezi Mungu waligundua hatari na madhara ya sigara kabla ya madaktari na wengineo. Sikiliza nini Imam Nurdiin A'Saalimi –Allah amrehemu- anasema kwenye

kitabu chake "*Jawhar A'nidhaam*" alichokitunga kabla ya karne moja iliyopita:

Bangi na afyuni* na tumbaku
Haramu kuvuta marufuku
Kwani maarufu vyalewesha
Kulewa ni fikra kuondosha
Yani akili kubadilisha
Hisabu hilo ni kulewesha
Kauli ya nyingine madh'hebu
Kwa hi tumbaku haikusibu
Wasema hili lalaza hali
Leweshi je iwapi akili
Na lengo la Sharia kwa hili
Ni kuhifadhi zetu akili
Lau haileweshi basi ni
Haramu dhara yake baini
Magonjwa mia na ishirini
Yaletwa kwayo wamebaini
Umanjano, kinywa yachachisha,
Na meno yasawidi jipasha
Kifua kikuu yasibisha
Na ini tumboni yatobosha

Mpaka akasema:

* Afyuni ni kasumba ya '*opium*'.

Yavunja nguvu ya kujamii
Na vingine vyote kama hii

Kalisema hilo pamoja na kuwa taathira ya sigara kwa nguvu ya kijinsia ilikuwa ni suala la mjadala na tafauti kati ya madaktari hadi wakati wa karibuni.

Baada ya kubainika ukweli na kuthibiti yaliyo thibiti katika madhara ya sigara kwa dalili zisizo shaka, tunawakuta maulama wanakaribia kukubaliana wote juu ya uharamu wa kuitumia, na hapana anaejadili juu ya hilo isipokuwa wachache. Kati ya walio kubaliana kuwa sigara ni haramu ni masheikh hawa watukufu:

1- Sheikh Jad Al-Haq Ali Jad Al Haq, Shekhe Mkuu wa Azhar – hayati.
2- Sheikh Muhammad Al Ghazali.
3- Dakta Yusuf Al Qaradhawi.
4- Dakta Nasr Farid Wasil.
5- Sheikh Abdul-Jalil Shalabi.
6- Sheikh Hamid Jaami'.
7- Sheikh Zakaria Al Barri.
8- Sheikh 'Atiyya Saqr.

9- Sheikh Mustafa Muhammad Al Hadidi A'tair.
10-Sheikh Abdalla Al Mushid.
11-Dakta Ahmad Umar Hashim.
12-Dakta Husaini Abdul-Majiid Hashim.
13-Sheikh Muhammad A'Zuhaili.
14-Sheikh Mahdi Abdul-Majiid Mustafa.

Na juu ya uharamu wa sigara imekubaliana Kamati ya Kudumu ya Tafiti za Kitaalamu na Fatwa ya Saudi Arabia.

Ama wale wachache wanaojadili hilo, mjadala wao hautokani ila na mapenzi ya kitu yaliyomo katika nafsi zao. Kwani wao ima ni washiriki wa sigara, hawawezi kuiacha, na kwa hiyo wanajaribu kutafuta uhalali wa kitendo chao hicho, au wana haja maalumu katika nafsi zao wanataka kuikidhi na hawana njia ya kuifikia ila fatwa yao hii.

Katika ya kustaajabisha niliyoona yamesemwa na baadhi ya hawa ni kule mmoja wao kudai kuwa sigara si haramu pamoja na kuwa anakubali kama ina madhara, akidai kuwa kuiharamisha sigara kutabidi yaharamishwe pia mafuta, uwanga na

vinginevyo katika vyakula vinavyodhuru kwa vile pia imethibiti kuwa vinadhuru. Na hii ni hoja potofu ya ajabu na ni kushindana na ukweli. Kwani wapi baina ya sigara na chakula!

"Hapana kitu itachokubali akili
iwapo mchana utahitaji dalili"

Chakula mtu hana budi nacho, na hilo linatafautiana kwa mujibu wa kazi yake na tabu yake. Na kila mmoja hana budi chakula chake kiwe mchanganyiko wa vitu vya uwanga na vya mafuta na venginevyo. Amenambia daktari mmoja mtaalamu wa lishe ('*dietitian*') kuwa chakula bora kwa mwanaadamu kiwe 59% kabohidrati (vyakula vya uwanga) na utembo (nyuzinyuzi au '*fibre*'), na 30% mafuta, na 11% protini; na kwamba wastani wa haja ya mwanadamu ya nguvu kwa siku ni kilokalori za joto 2300 kwa mwanamme aliyekwisha kuacha kazi, na 1900 kwa mwanamke aliyekwisha kuacha kazi, na 2200 kwa mke anayefanya kazi za nyumbani, na 2500 kwa karani wa ofisini mwanamme, na 2100 kwa karani wa ofisini mwanamke, na 3200 kwa mfanyakazi kiwandani mwanamme, na 2400 kwa mfanyakazi kiwandani mwanamke, na 3600 kwa mfanya kazi za mikono. Maana yake

vyakula hivo ni vya lazima kwa ajili ya uzima wa mwili na havidhuru vikiwa kwa kadiri ya haja yake, lakini madhara huja pakikiukwa mipaka ya wastani, na hilo halijuzu kisharia. Kwa ajili hiyo Mwenyezi Mungu Subhana ameamrisha kufanya kiasi katika kula na kunywa, akakataza kupindukia mipaka ya wastani katika mawili hayo aliposema:

﴿ وَكُلُواْ وَٱشۡرَبُواْ وَلَا تُسۡرِفُوٓاْۚ إِنَّهُۥ لَا يُحِبُّ ٱلۡمُسۡرِفِينَ ﴾

الأعراف: ٣١

{...na kuleni na kunyweni, na msitumie kwa fujo. Kwa hakika Yeye hawapendi wanao tumia kwa fujo} (Al-a'raaf: 31)

Ikiwa vitu hivi ni vya lazima kwa maisha ya mwanaadamu, vipi vitalinganishwa na kitu kiovu kama sigara, ambayo yote ni madhara na sumu zinazoua. Yatosha kubainisha hilo yaliyokuja katika "Muongozo wa Kiafya" kutoka Shirika la Afya la Dunia kupitia Ofisi yake ya Mashariki ya Kati, ambayo ni kama ifuatavyo: "Huenda ikawa katika yanayo hujumu kwa namna iliyo wazi kabisa afya ya mtu binafsi na ya jamii kwa jumla ni sigara. Kwani si siri ikiwa watu zaidi ya milioni nne duniani wanakufa kila

mwaka kwa maradhi ambayo msingi wake ni kuvuta sigara, kama saratani ya mapafu, uvimbe wa muda mrefu wa mianzi ya pumzi ('*chronic bronchitis*'), uvimbe wa mapafu, magonjwa ya mishipa ya damu ya moyo ('*coronary heart desease*'), na saratani ya kibofu cha mkojo. Haya yanamaanisha utokeaji wa vifo zaidi ya alfu 11 kila siku. Na katika yanayofaa kuzingatiwa kwamba hakuna ulimwenguni kote aliyeweza kuvumbua faida hata moja ya kuvuta sigara. Kwa hiyo tumbaku ni kitu chenye madhara matupu kwa mtu binafsi, familia yake na jamii yake. Na hili linaifanya tumbaku iwe kitu cha namna pekee kati ya vitu ambavyo wanaadamu wanavitumia kwa wingi ulimwenguni; maana hata ulevi Mwenyezi Mungu Subhana kausemea ifuatavyo:

﴿ يَسْـَٔلُونَكَ عَنِ ٱلْخَمْرِ وَٱلْمَيْسِرِ ۖ قُلْ فِيهِمَآ إِثْمٌ كَبِيرٌ وَمَنَٰفِعُ لِلنَّاسِ وَإِثْمُهُمَآ أَكْبَرُ مِن نَّفْعِهِمَا ﴾ البقرة: ٢١٩

{Wanakuuliza juu ya ulevi na kamari. Sema: Katika hivyo mna dhambi kubwa na manufaa kwa watu. Lakini dhambi zake ni kubwa zaidi kuliko manufaa yake} (Al-baqara: 219)

Unaona Mwenyezi Mungu jinsi alivotaja kuwepo baadhi ya manufaa katika ulevi, lakini ameuharamisha kikamilifu kwa kuwa madhara yake yamezidi manufaa yake; itakuwaje basi tumbaku, ambayo haina faida inayotajwa na mtu ye yote? Bali wavuta sigara wenyewe wanakubaliana kuwa inaleta maafa na mashaka."

Kutokana na haya inabainika kuwa wahanga wa sigara wanawazidi wahanga wa madawa ya kulevya kwa asilimia kubwa sana, na wanawazidi pia wahanga wa maradhi ya ukimwi. Juu ya yote hayo, pamoja na kukubaliana juu ya kupiga vita madawa ya kulevya na kuyawekea sharia kali, hata adhabu ya kufanya biashara ya madawa ya kulevya imefikia kifo katika baadhi ya nchi, tunaukuta ulimwengu unadharau kiasi hiki cha ajabu kwa upande wa sigara, hali ya kuwa kama ingefaa kuruhusu sigara basi ingefaa pia kuruhusu madawa ya kulevya, maana hakuna tafauti kati ya mawili haya. Isitoshe, ushiriki wa sigara ni njia mojawapo inayopeleka kwenye ushiriki wa madawa ya kulevya, kwasababu aina kadha za madawa ya kulevya zinatumiwa kwa njia ya

kuvuta kama tumbaku na kwa kutumia sigara ambazo hazitafautiani sana na sigara za tumbaku. Mpingano gani huu ulio wazi kabisa unaofanywa na ulimwengu wa leo, ikiwa unaregeza kamba na kufungua milango na kusafisha njia ili sigara zienee na kutangaa hali ya kuwa zinateketeza mimea na vizazi na kuangamiza vichanga na vipevu, wakati ambapo unapiga vita vikali bila huruma madawa ya kulevya?!

Jawabu ya Ibara ya Pili:

Kila kinacho dhuru ni haramu hata kikiwa mti unaomea, na kwa hiyo vitu hivi vinavyo lewesha vimekuwa haramu kisharia, na mataifa yote yamekubaliana kuvipiga vita, hata wasiokuwa na dini, pamoja na kuwa ni miongoni mwa mimea. Kwa ajili hiyo mmea wa tumbaku ni haramu haijuzu kuutumia kwa hali yo yote. Na imethibiti kutokana na kauli ya madaktari wataalamu kuwa tumbaku haina manufaa yo yote, na kwa hiyo hakuna sababu ya kuihalalisha itumike kwa hali yo yote. Kweli, lau kama itathibiti kuwa inafaa kwa kutibia majeraha, mfano kwa kuipaka juu yake bila hilo kusababisha madhara basi itajuzu wakati huo

kutumia manufaa yake kwa sharti madhara yake yaepukwe, kwasababu manufaa yote asili yake ni kuhalalishwa, kutokana na kauli Yake Taala:

﴿ هُوَ ٱلَّذِى خَلَقَ لَكُم مَّا فِى ٱلْأَرْضِ جَمِيعًا ﴾

البقرة: ٢٩

{Yeye ndiye aliye kuumbieni vilivyomo katika ardhi vyote} (Al-baqara: 29)

Jawabu ya Ibara ya Tatu:

Kuongeza kitu kilicho haramishwa katika tumbaku kunazidisha uharamu wa tumbaku wakati imesha bainika kuwa tumbaku yenyewe ni haramu kutokana na kuthibiti madhara yake na taathira yake mbaya.

Jawabu ya Ibara ya Nne:

Kuhalalisha haramu na kuharamisha halali, kila moja kati ya mawili hayo ni kosa kubwa si dogo, kwasababu ni kumzulia uwongo Mwenyezi Mungu, wakati Mwenyezi Mungu Taala kasema:

﴿ وَلَا تَقُولُواْ لِمَا تَصِفُ أَلۡسِنَتُكُمُ ٱلۡكَذِبَ هَٰذَا حَلَٰلٞ وَهَٰذَا حَرَامٞ لِّتَفۡتَرُواْ عَلَى ٱللَّهِ ٱلۡكَذِبَۚ إِنَّ ٱلَّذِينَ يَفۡتَرُونَ عَلَى ٱللَّهِ ٱلۡكَذِبَ لَا يُفۡلِحُونَ ﴾ النحل: ١١٦

{Wala msiseme uwongo, kwa kuropokwa na ndimi zenu: Hichi halali, na hichi haramu – mkamzulia uwongo Mwenyezi Mungu. Hakika wanao mzulia uwongo Mwenyezi Mungu hawatafanikiwa} (A'nahl: 116)

Pia kasema:

﴿ قُلۡ أَرَءَيۡتُم مَّآ أَنزَلَ ٱللَّهُ لَكُم مِّن رِّزۡقٖ فَجَعَلۡتُم مِّنۡهُ حَرَامٗا وَحَلَٰلٗا قُلۡ ءَآللَّهُ أَذِنَ لَكُمۡۖ أَمۡ عَلَى ٱللَّهِ تَفۡتَرُونَ ﴾

يونس: ٥٩

{ Sema: "Je, mnaonaje zile riziki alizo kuteremshieni Mwenyezi Mungu kisha mkafanya – katika hizo – (nyengine kuwa za) haramu na (nyengine kuwa za) halali." Sema: "Je, Mwenyezi Mungu amekuruhusuni (kufanya hivyo) au mnamzulia Mwenyezi Mungu uwongo tu?"} (Yunus: 59)

Kisha Mwenyezi Mungu kaambatisha jambo la kuharamisha halali na kumshirikisha Yeye,

akalihisabu miongoni mwa sifa za washirikina aliposema:

﴿ سَيَقُولُ ٱلَّذِينَ أَشۡرَكُواْ لَوۡ شَآءَ ٱللَّهُ مَآ أَشۡرَكۡنَا وَلَآ ءَابَآؤُنَا وَلَا حَرَّمۡنَا مِن شَيۡءٖ ﴾ الأنعام: ١٤٨

{Watasema walio shirikisha: Lau Mwenyezi Mungu ange taka tusingeli shirikisha sisi, wala baba zetu; wala tusingeli haramisha kitu chochote} (Al-an-'aam: 148)

Vile vile kasema:

﴿ وَقَالَ ٱلَّذِينَ أَشۡرَكُواْ لَوۡ شَآءَ ٱللَّهُ مَا عَبَدۡنَا مِن دُونِهِۦ مِن شَيۡءٖ نَّحۡنُ وَلَآ ءَابَآؤُنَا وَلَا حَرَّمۡنَا مِن دُونِهِۦ مِن شَيۡءٖۚ كَذَٰلِكَ فَعَلَ ٱلَّذِينَ مِن قَبۡلِهِمۡ ﴾ النحل: ٣٥

{Na washirikina wamesema: Mwenyezi Mungu angeli taka tusingeliabudu chochote badala yake, sisi wala baba zetu, wala tusingeli haramisha chochote bila ya Yeye. Kama hivyo walifanya walio kuwa kabla yao} (A'nahl: 35)

Tena kuharamisha kwa makusudi kile ambacho uhalali wake umethibiti kwa andiko la Sharia lilo wazi na lisilo shaka ni katika kufuru

ya kumshirikisha Mwenyezi Mungu inayomtoa mtu katika Dini. Mfano wake ni kama kuharamisha ndoa, biashara, na kula, kunywa na kuvaa bila fujo wala majivuno. Halikadhalika kuhalalisha kile ambacho andiko la Sharia lilo wazi na lisilo shaka limeonesha kuwa ni haramu, kama kuzini, ulevi, kamari, kuua nafsi iliyo haramu kuuliwa bila haki, kuua watoto kwa ujinga bila kujua, kuwaasi wazazi na kuwatupa jamaa.

Vile vile kumsemea Mwenyezi Mungu usilolijua, hili peke yake ni katika makosa makubwa hata kama msemaji atasudufia kusibu ukweli katika analosema; kwani Mwenyezi Mungu ameliambatisha hilo pia na kumshirikisha aliposema:

﴿ قُلۡ إِنَّمَا حَرَّمَ رَبِّيَ ٱلۡفَوَٰحِشَ مَا ظَهَرَ مِنۡهَا وَمَا بَطَنَ وَٱلۡإِثۡمَ وَٱلۡبَغۡيَ بِغَيۡرِ ٱلۡحَقِّ وَأَن تُشۡرِكُواْ بِٱللَّهِ مَا لَمۡ يُنَزِّلۡ بِهِۦ سُلۡطَٰنٗا وَأَن تَقُولُواْ عَلَى ٱللَّهِ مَا لَا تَعۡلَمُونَ ﴾ الأعراف: ٣٣

{Sema: alichoharamisha Mola wangu ni mambo machafu ya dhahiri na ya siri, na dhambi, na uasi (wa viongozi) bila ya haki, na

kumshirikisha Mwenyezi Mungu na asicho kiletea uthibitisho, na kumsemea Mwenyezi Mungu msiyo yajua} (Al-a'raaf: 33)
Hilo ni katika ambayo Shaitani anawaamrisha watu ili awapoteze; na Mwenyezi Mungu Subhana kasema:

﴿ إِنَّمَا يَأۡمُرُكُم بِٱلسُّوٓءِ وَٱلۡفَحۡشَآءِ وَأَن تَقُولُواْ عَلَى ٱللَّهِ مَا لَا تَعۡلَمُونَ ﴾ البقرة: ١٦٩

{Yeye (Shaitani) anakuamrisheni maovu na machafu, na mumsemee Mwenyezi Mungu yale msiyo yajua} (Al-baqara: 169)

Haya ndiyo niliyowahi kuyakumbuka katika kujibu masuali uliyouliza ewe ndugu mtukufu. Namuomba Allah anipe mimi na wewe na kila Muislamu mafanikio ya kutenda kila apendalo na kuridhia, na atukinge na kila achukialo na kulikana! Wassalaamu alaykum warahmatu'LLahi wabarakaatuh.

Ahmed bin Hamed Al Khalili
26 Rajab, 1424H